# Mwongozo wa Kukuza "Uwazi" na Kuepusha Rushwa

## Wajibu na Wito

**Mwongozo huu wa kukuza "uwazi" na kuepusha rushwa unaweka wajibu kwa vyombo vyote vilivyoridhia makubaliano haya. Mwongozo huu pia unaweka wazi viwango vya chini vya utekelezaji wa mwongozo huu, ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya hatua zipi zifuatwe katika kuhakikisha utekelezaji unakuwepo.**

**Ni muhimu mwongozo huu uwasilishwe kwa washirika, makanisa wanachama na katika jamii na jambo hili lifanyike katika njia sahihi. Kuuelewa mwongozo huu na kufikia makubaliano juu yake ni jambo litakalohusu pande zote husika.**

**Kwa misingi ya mwongozo huu, mashirika yanawajibika kuandaa, kurekebisha na kuboresha miongozo yao ya kimaadili iliyopo. Mwongozo huu unawalenga wafanyakazi wa kawaida na wale wa kujitolea. Wawakilishi katika ngazi za juu hasa viongozi wanabeba jukumu la kuwa mfano bora katika utekelezaji wa mwongozo huu.**

## Utangulizi

***"Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana, kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu." (1 Petro 4,10)***

Kwa njia ya Yesu Kristo sisi ni sehemu ya Mungu, na kwa njia ya Roho Mtakafitu Mungu anatuzawadia kuwa sehemu ya ushirika wake. Kwa maana hiyo sisi tu sehemu ya Misioni (*Mission*) ya Mungu. Ni kwa njia hii pia tunaalikwa kuwa na ukamilifu wa maisha. Ukamilifu huu unaonekana pale tutakaposhirikishana sisi kwa sisi – jinsi tulivyo, na kushirikiana katika vitu tulivyonavyo. Hii ina maana pia kuwa sisi sote ni watoaji na wapokeaji. Hata hivyo wajibu na majukumu yetu ni pamoja na:

- kuheshimu hadhi na utu wa mtu
- Kujitoa kusikolenga faida binafsi na uwepo wa hali ya kuaminiana katika matumizi ya fedha na rasilimali kwa kuzingatia mambo yaliyokusudiwa
- Kuwa na ujasiri wa kukubali mabadiliko na kurekebisha makosa.
- Kuwa na matumaini bila kukata tamaa, licha ya kuwepo vipingamizi.

***"Ye yote aliye mwaminifu katika mambo madogo, pia ni mwaminifu hata katika mambo makubwa, naye mtu ambaye si mwaminifu katika mambo madogo pia si mwaminifu katika mambo makubwa. Nanyi kama hamkuwa waaminifu na mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe? (Lk 16, 10,12)***

Sisi sote tu washirika katika kazi ya misioni ya Mungu. Hivyo kwa pamoja au katika hali binafsi tunabeba wajibu katika kufanikisha au kutofanikisha ushirikiano wetu.

Mali tulizokabidhiwa, uzoefu, ujuzi na matumaini tuliyonayo si kwa mahitaji yetu binafsi tu. Ndio maana tunaahidiana "uwazi" na kushiriki katika mapambano ya pamoja dhidi ya aina zote za ubadhilifu, matumizi mabaya ya fedha na rushwa. Kwa maana tunajua kukiwa na mpangilio mzuri na kuwajibishana - "Kila kitu kimefunuliwa na kiko wazi mbele ya macho ya Mungu, ambaye tutalazimika kutoa hesabu mbele yake" *(Ebr. 4:13).*

### *"Usipokee rushwa, kwa kuwa rushwa hupofusha wale waonao na kupinga maneno ya wenye haki.(Kutoka 23,8)*

Vitendo vya rushwa vimekataliwa tangu mwanzo, hata chini ya mapokeo na sheria katika biblia. Mungu mwenywe amejionyesha kuwa hawezi kuhongwa, "...ambaye hana upendeleo na hapokei rushwa, na huwapigania yatima na wajane, humpenda mgeni akimpa chakula na mavazi." (*Kumb.10.17b-18).* Kwa hiyo kujipatia sifa na faida binafsi kwa gharama za mtu mwigine ni jambo ambalo linapingana na misingi ya kibiblia, misingi ambayo sisi tunawiwa kuifuata. Kwa kutilia maanani wajibu huu Kanisa la Yesu Kristo linakuza na kuhamasisha hali ya "uwazi", uwajibikaji na uadilifu katika umoja wake wa kiekumene, haya yakifanyika kwa ufahamu wote na dhamiri safi.

Rushwa si swala la mmomonyoko wa maadili tu. Rushwa humwondelea mtu hadhi na utu wake, na ni kikwazo kwa maaendeleo katika jamii. Maisha huharibika kupitia vitendo vya rushwa. Pia haki za wasiojiweza kijamii hudidimizwa na ukuaji wa uchumi hukwamishwa maana katika mazingira ya rushwa utaratibu na amri ya haki (fairness) havifuatwi. Rushwa hudhoofisha imani na uaminifu, huvuruga pia uwazi na uwezo wa kuwa na maono sahihi ya mbeleni. Uwepo wa rushwa unakuza unyanyasaji.

Rushwa sio jambo geni na jambo la hivihivi tu. Sababu na vyanzo vyake ni wazi na vyenye sura mbalimbali. Ni pamoja na uroho wa fedha na madaraka, woga wa kupoteza sifa na heshima na kutokuwa na hali nzuri ya kimaisha. Sababu hizi huweza kuifanya dhamiri ya mtu kufa au kuwa huru kijihusiha na matendo ya rushwa - jambo ambalo kimsingi hushusha hadhi ya imani ya mtu husika kama mkristo.

Kwa kutambua neema na huruma za Mungu, kanisa halimhukumu mtu kwa matendo aliyoyafanya, hata hivyo kanisa linalo jukumu la kuweka wazi matendo ya rushwa na kuyarekebisha. Ndio maana ni muhimu kuwepo kwa kanuni na maelekezo wazi ambayo yatakuwa kama mwongozo katika kukabiliana na vitendo vya rushwa, hizi zaweza kuwa kanuni zinazoongoza utendaji wa mtu binafsi au makanisa na mashirika.

### *"...ulimwenguni mtapata dhiki; Lakini jipeni moyo, kwa maana mimi nimeushinda ulimwengu.'' (Yohana 16: 33)*

Utayari wa kuhakisha uwepo wa "uwazi" na mapambano dhidi ya rushwa ni vitu ambavyo vinahitaji ujasiri mkubwa. Maana mahusiano ya karibu yakichezewa au kuvunjwa yanaweza kuwa jambo la kuogopesha au linaloweza kusababisha tabia zisizokubalika kwa pande husika.

Uwajibikaji wa namna hii (katika kutetea "uwazi" na kupinga rushwa) unaliimarisha kanisa na washarika wake katika wito wake wa kinabii. Katika umoja wa kikristo amani kwa maana ya "Shalom" humaanisha pia kutokuwa na hofu katika kukiri makosa binafsi, maana kwa kufanya hivyo hakuondoi umoja wa kindugu uliopo katika kristo. Mashirika ya kikristo/kikanisa na washirika wake wote wanapaswa kuwa mfano katika kulitekeleza jambo hili. Ndio maana mashirika ya kikristo/kakanisa yanawajibika kwa pamoja/chini ya mwavuli wa **EMW (Evangelisches Missionswerk in Deutschland** – Chama cha huduma na/za Mission cha makanisa ya kiprotestanti ya Ujerumani) kuwa na matumizi mema ya mali na fedha wanazomiliki na walizokabidhiwa. Ndio maana mashirika haya pamoja na washirika wake kwa pamoja wanalenga kufikia makubaliano katika kanuni zifuatazo:

## "Uwazi" kama njia kuu ya kuepukana na rushwa

Mambo yote na hasa yanayohusu matumizi ya fedha ni lazima yafanyike kwa uwazi. Yaani uwazi kati ya wafanyakazi wote, kamati husika, vyombo vya uwakilishi, makanisa wanachama, washirika husika, walengwa wa misaada na wafadhili wote – wale waliojitoa kupitia kanisani na wale ambao misaada yao haikupitia kanisani.

Dhana hii ya "Uwazi" tunaitafsiri kama hali nzima ya utoaji wa taarifa zinazojitosheleza na uwajibikaji. Hali hii huhitaji kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa uwazi kati ya pande husika, hata wakati ambao shida inaonekana kuwepo. Katika mambo yahusuyo fedha hali hii humaanisha utoaji wa ripoti (za fedha) zilizo wazi. Hii inamaanisha pia uwezo wa kusema ukweli wa matumizi ya amana zilizowekwa kwetu. Katika mambo yahusuyo mipango na usimamizi hali hii ya uwazi inamaanisha kufuata miundo, mifumo na kanuni zilizowekwa kwa uaminifu. Hili linahusu pia taratibu sahihi za kuomba na kutoa fedha, uandishi sahihi wa taarifa za fedha na mawasiliano kwa ujumla. Hii inajumuisha pia kusimimia matumizi sahihi yanayolenga makusudio ya awali yaliyowekwa. Ni muhimu pia kuepukana na migogoro ya kimaslahi (conflict of interest). Hata hivyo migogoro hii inapogunduliwa iwekwe wazi, na wahusika wachukuliwa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kupumzishwa au kuachia kabisa madaraka au nafasi husika. Juhudi hizi huwa za mafaniko kunapokuwepo na utaratibu mzuri wa udhibiti na usimazi katika mambo husika, utaratibu ambao pia unatoa nafasi ya kushiriki ipasavyo kwa washirika na makundi yote husika.

Rushwa ni tatizo linalotakiwa kuepukwa katika ngazi zote. Dhana hii ya "Rushwa" tunaitafsiri kama kila hali ambayo mtu hutafuta faida binafsi au hutafuta kumfaidisha mtu mwigine kupitia matumizi mabaya ya madaraka au fedha mtu alizokabidhiwa kutoka kwenye vyombo vya umma na vile visivyokuwa vya umma.

Uwepo wa rushwa huharibu umoja wa kundi lengwa na pia unashusha sifa za washiriki wote. Licha ya hilo rushwa pia inakiuka matakwa ya mtoaji na mpokeaji wa msaada.

Panapokua na tuhuma za rushwa za msingi ni lazima utarabitu sahihi wa kisheria uliowekwa ufuatwe. Ikithibitika kisheria kuwa ni rushwa matokea haya yanapaswa yawekwe wazi na mhusika awajibishwe kulingana na sheria za kanisa na nchi husika, na lisiishie hivihivi bila hatua stahiki.

## Hatua za kuzia Rushwa

Hatua za kuzuia rushwa za awali na za msingi katika utendaji zinapaswa kwa ujumla zifikiwe kwamba:

- Uhamisho wa fedha, uendeshaji wa miradi pamoja na kubadilishana kwa wafanyakazi kunafanyika kwa makubaliano na kimaandishi kati ya washirika na makanisa wanachama kwa kuzigatia viwango vya mongozo huu.
- Wahusika, yaani wafanyakazi wanaohusika katika maswala muhimu ya kifedha kama vile maamuzi ya utoaji fedha, utoaji zabuni nk. lazima wawe watu tofauti na wenye majukumu tofauti. Hali hii inalenga kuondoa hali ya kuwa na watu wale wale katika hatua zote za kifedha.
- Uwezo wa kiutawala na uongozi unapimwa kwa kuzingatia kama uongozi unafaa na kama unajitosheleza. Inategemewa pia kuwa kwa njia ya mafunzo uwezo huu utaboreshwa.
- Wafanyakazi wote pamoja na wale wanaojitolea wanawajibika chini ya kanuni za maadili ya shirika au kanisa husika. Hili ni swala la kuzingatiwa na kuwekwa kimaandishi.
- Upokeaji wa zawadi na mali nyingine zilizoko juu ya kiwango cha kawaida cha mazingira husika ni jambo lisilokubalika.
- Matendo yanayoashiria uvunjifu wa sheria lazima yafikishwe kwenye vyombo vya sheria husika.

**Yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa katika Sekta ya fedha:**

- Maswala yote yahusuyo malipo ya Fedha lazima yafanyike chini ya kanuni ya "macho manne" – "Vieraugenprinzip". Kanuni hii inasema maamuzi muhimu yasifanywe na mtu mmoja. Inapobidi kufanya kinyume na kanuni hii, ni lazima chombo au mtu husika kutaarifiwa kimaandishi na chombo au mtu husika kutoa ruhusa pia kimaandishi.
- Mahesabu ya fedha lazima yafanyike kwa mujibu wa viwango vya kitaifa au hata kimataifa. (Kwa mfano kwa kufuata sheria za Kanisa, taratibu za ukaguzi wa ndani ya Kanisa pamoja na zile za nchi husika zinaweka wazi makubaliano ya matumizi ya fedha na misingi ya uwajibikaji). Ni muhimu kuwepo wakaguzi wa mahesabu walioteuliwa wanaokuja mara kwa mara kukagua hali nzima ya utunzaji wa fedha.
- Ni muhimu kuwepo ukaguzi na udhibiti wa ndani, mfano ukaguzi wa ghafla kwenye vitabu vya fedha, hundi na matumizi madogomadogo.
- Taratibu na maswala yote ya kiofisi yanayohusu fedha kama vile mikataba ya manunuzi na huduma, bili na mikataba ya kazi n.k. lazima yafanyike kwa maandishi.

**Mambo mengine ya kuzingatiwa:**

- Ni muhimu kubainisha mazingira na maeneo yanayopelekea mwanya wa rushwa - ikiwezekana lifanyike kitaalam (risk analysis*)*. Hii itasadia kwamba kila hatua itakayokuwa inachukuliwa kunalenga aina na ukubwa wa hatari inayoonekana kujitokeza. Baada ya kubainisha idara zenye kutoa nafasi

kubwa ya kukaribisha rushwa, kuwepo na mzunguko wa wafanyakazi katika idara hizo kwa muda maalum.

- Wakuu wa idara za fedha wa mashirika, makanisa wanachama pamoja na washirika (wadau) waungane kwa pamoja na kutengeneza miongozo. Lakini pia washiriki katika warsha, mafunzo na kozi mbalimbali zinazoweza kuwasaidia katika utendaji kazi wao.
- Kuwepo na kanuni na taratibu zinazopinga matumizi mabaya ya ofisi au undugu, (mfano katika kupata nafasi za kazi, upendeleo katika kutoa udhamini wa masomo, kuweka ukomo wa muda wa kukaa madarakani na kanuni nyingine dhidi ya upendeleo).

**Hatua za uchunguzi wa kesi za rushwa**

- Taarifa kuhusu tuhuma za rushwa zinaweza kupatikana kwa njia ya ukaguzi, lakini pia hata kwa njia nyingine. Mtu yeyote mwenye kupata habari juu ya vitendo vya rushwa anao wajibu wa kutoa taarifa hizo kwa mkuu wake wa kazi, ambaye naye anao wajibu wa kufikisha taarifa hizo kwenye vyombo vya utawala. Uwepo wa misingi ya utaratibu huu wa utoaji taarifa ni muhimu.
- Ni vyema kuwepo na utaratibu wa uteuzi wa "Ombudsmen" – (wachunguzi maalumu) au kamati itakayoshughulikia mambo ya rushwa. Kamati hii haitoi ulinzi kwa mtoa taarifa ("whistle blower")tu, bali hufanya kazi kama chombo huru wakati wa kushughulikia kesi za rushwa. Mtoa taarifa pia anaweza kurejea kwa "Ombudsmen" au kamati hiyo husika atakapohisi kuwa kwa kutimiza wajibu wake wa kutoa taarifa anaweza kujisababishia matatizo (mfano kuhamishwa au kuonewa katika mazingira yake ya kazi).
- Kuwepo na utaratibu mzuri wa kufanya uchunguzi ili kupata taarifa sahihi , ikiwa ni pamoja na hakikisho la ulinzi na usalama wa watoa habari. "Ombudsmen" au kamati teule itakuwa tayari kila mtu kwa kila wakati, vyombo hivi lazima pia vitambuliwe na vijulikane kwa wafanyakazi.
- Wafanyakazi wa kudumu hawaruhusiwi kushikilia nafasi ya "Ombudsmen". Kama kazi ya uchunguzi itafanywa na kamati basi kamati hiyo itaundwa na wanakamati ambao si wafanyakazi. Nafasi hizo ni za wafanyakazi wa kujitolea pamoja na watu wa nje. Katika utendaji vyombo hivyo vinatakiwa kupewa ushirikiano kutoka kwa mashirika ya kikanisa na makanisa wanachama pamoja na washirika wengine.
- Inashauriwa na kupendekezwa kuwepo kwa **"Kikundi kazi" – „Task Force"** cha kufanya uchunguzi kwenye mashirika makubwa. Lengo lake ni kuwa na watu wenye kufikisha mapendekezo kwenye ngazi za uongozi na kutoa taarifa kwa wale wafanyakazi wasioshiriki katika uchunguzi wa kesi za rushwa. Ni wazi kuwa uchunguzi wa tuhuma za rushwa si jambo rahisi. Katika hatua za uchunguzi wahusika au mhusika wa kesi hatakiwi kushirikishwa.

  Maamuzi ya busara na ushiriki thabiti **(commitment)** ni muhimu sana katika uchunguzi wa kesi za namna hii. Ni muhimu pia kuwepo na makubaliano ya nani au kamati gani itakayo kuwa na jukumu la kutoa adhabu pamoja na kutoa taarifa kwa umma juu ya kesi ya rushwa husika.

Evangelisches Missionswerk
in Deutschland

Association of Protestant Churches
and Missions in Germany

## Adhabu (Sanktionen)

Ikiwa rushwa itadhibitika mhusika atapaswa kuchukuliwa hatua zinazostahili. Hatua sahihi zitapaswa pia kuchukuliwa kwa taarifa za rushwa zilizotolewa isivyosahihi, kwa makusidi binafsi au mabaya. Kwa hivyo kuna adhabu ambazo zinaweza kuchukuliwa dhidi ya mtu binafsi na zile ambazo zinaweza kuchukuliwa dhidi ya taasisi.

**Hatua zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya mtu binafsi ni:**

- Adhabu za kikazi, mfano kuonywa , kuachishwa kazi kwa kufuata taratibu za kisheria, kuachishwa kazi ghafla au hatua nyingi za kinidhamu zenye matokeo tofauti kama vile kukatwa pension n.k.
- Kuondolewa katika nafasi au madaraka husika kwa wale wanaofanya kwa kujitolea, kuchaguliwa au kuitwa.
- Kulipia hasara iliyotokea kutoka kwenye mfuko binafsi, mfano kwa njia ya kukatwa mshara.
- Kuchukuliwa hatua za kisheria

**Hatua zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya taasisi**

- Kupunguza au kutotoa msaada wa kifedha hadi tuhuma za rushwa zitakapofafanuliwa
- Kufidia ubadhilifu uliojitokeza kwa kutumia mafungu mengine tofauti ya fedha (mfano Block Grants na fedha za miradi)
- Mashirika husika kubaliana aina za adhabu ambazo zitapaswa kutolewa, mfano adhabu ya kulipa fidia kwa kosa, adhabu ambazo zinaweza kuhusu makato katika mafungu, au adhabu nyingine ambazo zinaendana na malengo ya awali yaliyokuwa yamekusudiwa.
- Katika mazingira hatarishi kuvunjwa ushirikiano

Adhabu zitatolewa kwa uangalifu mkubwa. Hata hivyo makali ya adhabu hizi yatafikiwa pale patakapokosekana nia ya thati ya ushirikiano kufikia „uwazi", kuzuia uchunguzi au mausala ya rushwa yatakayothibitika.

## Uhusiano na umma

Katika hatua za kukuza "uwazi" na kuepusha rushwa uhusiano na umma (public relations) una nafasi muhimu. Ndio maana mambo yafuatayo ni muhimu na ya kuzingatiwa :

- Uwajibikaji uonekane wazi , mf. katika *website* na repoti za mwaka
- Kusisitiza na kukumbusha kanuni za maadili
- Utii wa kanuni za msingi na uwepo wa mawasiliano mazuri
- Kutoa taarifa za kutosha kuhusu kesi na tuhuma za rushwa
- Uwepo wa utaratibu unaoeleweka wenye kushughulikia kesi na tuhuma za rushwa, uwepo wa mipango ya kuhakisha uwepo wa uwajibikaji (iwe ni mipango yenye kufaa na yenye kulenga makundi husika , kama vile wafadhili, washirika na vyombo vya habari).
- Kuzingatiwa kwa haki za watu binafsi na "haki ya faragha" katika kutimiza wajibu wa kutoa habari.

Hamburg, May 2012